JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA NNE

KIKAO CHA TANO

01 SEPTEMBA, 2026

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

____

MKUTANO WA NNE

KIKAO CHA TANO – TAREHE 01 SEPTEMBA, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI MKUU:

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na. 13 la tarehe 27 Machi, 2026;
2. Toleo Na. 14 la tarehe 03 Aprili, 2026;
3. Toleo Na. 15 la tarehe 10 Aprili, 2026;
4. Toleo Na. 16 la tarehe 17 Aprili, 2026;
5. Toleo Na. 17 la tarehe 24 Aprili, 2026;
6. Toleo Na. 18 la tarehe 01 Mei, 2026;
7. Toleo Na. 19 la tarehe 08 Mei, 2026;
8. Toleo Na. 20 la tarehe 15 Mei, 2026;
9. Toleo Na. 21 la tarehe 22 Mei, 2026;

10. Toleo Na. 22 la tarehe 29 Mei, 2026;
11. Toleo Na. 23 la tarehe 05 Juni, 2026;
12. Toleo Na. 24 la tarehe 12 Juni, 2026;
13. Toleo Na. 25 la tarehe 19 Juni, 2026;
14. Toleo Na. 26 la tarehe 26 Juni, 2026;
15. Toleo Na. 27 la tarehe 03 Julai, 2026;
16. Toleo Na. 28 la tarehe 10 Julai, 2026;
17. Toleo Na. 29 la tarehe 17 Julai, 2026;
18. Toleo Na. 30 la tarehe 24 Julai, 2026;
19. Toleo Na. 31 la tarehe 31 Julai, 2026;
20. Toleo Na. 32 la tarehe 07 Agosti, 2026;
21. Toleo Na. 33 la tarehe 14 Agosti, 2026;
22. Toleo Na. 34 la tarehe 21 Agosti, 2026;

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa Mwaka 2026 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2026].*

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali wa Mwaka 2026 [The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2026].

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

56. MHESHIMIWA KAKULU BURCHARD KAKULU (MBAGALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Shule ya Msingi Mitaa ya Barabara ya Mwinyi Kata ya Kiburugwa – Mbagala.

57. MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA (KALENGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha ili kukamilisha ukarabati wa Shule Kongwe ya Sekondari Tosamaganga ambao ulishaanza.

58. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA (MBINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Myangayanga Kata ya Myangayanga katika Jimbo la Mbinga Mjini.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

59. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha Taaluma na kazi ya Udereva ina kuwa na staha, hadhi na heshima sawa na Kada nyingine.

60. MHESHIMIWA DKT. EMMANUEL QAMBAJI NUWAS (MBULU VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutambua kwenye Muundo wa Utumishi wa Umma Wataalam wa Kada ya Afya wenye elimu ngazi ya Ubobezi.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

61. MHESHIMIWA RASHID HABIB ALI (MTAMBWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa suala la Mafuta na Gesi kwenye orodha ya Masuala ya Muungano.

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

62. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itaweka Mkongo wa Mawasiliano Kijiji cha Ipole Wilaya ya Tabora hadi Kata ya Inyonga Wilaya ya Mlele kwani eneo hili lina Wanyama wakali.

WIZARA YA UCHUKUZI:

63. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Meli Ukanda wa Pwani ili iweze kuunganisha nchi yetu na nchi jirani.

WIZARA YA NISHATI:

64. MHESHIMIWA EXAUD SILAONEKA KIGAHE (MUFINDI KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Mkataba wa kusambaza Umeme kutoka Mwenga *Power* kwenda Tanesco utabadilishwa ili Mwenga *Power* wabaki kuwa wazalishaji tu.

WIZARA YA KILIMO:

65. MHESHIMIWA EMMANUEL PETER CHEREHANI (USHETU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, upi mkakati wa kushughulikia bei ya pembejeo ambayo ipo juu tofauti na gharama za uzalishaji ikizingatiwa kuwa bei ya tumbaku imeshuka.

66. MHESHIMIWA ASHA SALUM MOTTO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kusambaza Matrekta Elfu Kumi katika Vijiji vyote nchini.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

67. MHESHIMIWA EDIFONSI JOAKIM KANONI (KALAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itafanya utafiti Ziwa Tanganyika ili kujua wingi wa Samaki.

68. MHESHIMIWA MWANTUMU MZAMILU ZODO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya maji katika maeneo ya Malisho ya Mifugo – Handeni.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

69. MHESHIMIWA FADHILI FABIAN NGAJILO (IRINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Gereza Kuu la Iringa litahamishiwa eneo la Mlolo Kata ya Isakalilo ili kupisha upanuzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa.

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

70. MHESHIMIWA NASSORO RASHID NASSORO (KONDE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Kambi ya JWTZ iliyopo Konde Kiperani yenye miaka zaidi ya 30 bila maboresho yoyote.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

71. MHESHIMIWA FATMA ALLY REMBO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia Wanawake Mafunzo ya Kimkakati ya Ufundi Stadi ili kuwawezesha kuibua fursa za kibiashara.

WIZARA YA MAJI:

72. MHESHIMIWA JOSEPH ENOCK TAMA (KALIUA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha Mradi wa kutoa Maji ya Ziwa Victoria kupeleka Jimbo la Kaliua ili wananchi wanufaike na Mradi huo.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

73. MHESHIMIWA ENG. RAMADHANI HAMZA SINGANO (BUMBULI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini Serikali itaongeza uwezo wa Kiwanda cha Mponde ambacho ni tegemeo katika kukuza uchumi na pato la Halmashauri ya Bumbuli.

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2026].*

DODOMA **BARAKA I. LEONARD**
01 SEPTEMBA, 2026 **KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA